

SOMO LA KUSIFU NA KUABUDU

1. UTANGULIZI

Kama isivyo muhimu kuenenda kupeleka injili ulimwenguni na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wa Yesu, ndivyo ilvyo muhimu kufundisha kuyashika yote asiyotuamuru Bwana yesu (*Mat28:19-20, Mk16:15-16, Kol3:16*) kufundisha na kuonyana.

Somo la kusifu na kuabudu ni muhimu kufundishwa ili kusifu na kuabudu kufanyike kulingana na maelekezo ya Biblia. *Hii itasaidia kupata matokeo sahihi ya ibada ya watu wa Mungu.* Tunahitaji maarifa (*Mt12:1*) mafundisho huleta maarifa, Biblia inatuonya kwamba tusifanye mambo bila maarifa (*Hos4:6*), Mungu hutufundisha tupate faida na kuongoza njia itupasayo kuifuata (*Isa48:17*). Tusipokuwa na maarifa hatutagundua mbinu za Shetani na mawakala wake wanavyojipenyeza kama malaika wa nuru na hivyo tutasifu na kuabudu isivyo sahihi (*2Kor11:14*).

2. ISTILAHİ NA MARAÑA ZAKE:

A. KUSIFU MARAÑA ZAKE NINI?

Kusifuni ni kuelezea kitu kilivyo kwa uzuri (*Kwa lugha rahisi-kunena vema juu ya kitu/mtu au nafsi*). Sifa zinaweza kuelekezwa kwa Mungu au mtu, mwajiri, mwana familia, mtumishi, rafiki, kitu/vitu, n.k.

Kumsifu Mungu kunahusu nafsi ya kila mwenye pumzi (*Zab 146:1-2; 150:6*) yaani mtaji wa kusifu Mungu ni pumzi ya uhai wako tu:

- Kumwelezea Mungu jinsi alivyo, tabia zake, Ukuu wake, matendo yake n.k.
- Kuelezea kwa furaha yale yote ambayo Mungu ameyafanya kweko. Kusifu Mungu kunahusiana kwa karibu na kutoa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya matendo yake makuu. Kusifu hakuhitaji chochote Zaidi yakuelezea kwa moyo wa ndani/kwa dhati kuhusu matendo ya haki yaliyotendwa na Mungu juu ya anayesifu. Katika muktadha huu, Mungu ndiye anastahili kusifiwa (*Zab18:3 ,63:5, 150:1-5, Heb43:15, 1Pet2:9*).

Nani Wanahusika Katika Kumsifu Mungu?:

- Mbingu na vyote ikiwa ni pamoja na Malaika (*Zab89:5-6, 103:20, 148:2, Lk2:13-14*) wakati Yesu Kristo amezaliwa Malaika walisisfu-[Atukuzwe Mungu juu mbinguni...]
- Wafalme na wakazi wote wa dunia (*Zab 138:4, 117:1-2, 150:6, Rm15:11*)

Mambo Muhimu Katika Kusifu

Mungu anweza kusifiwa kwa:

- *Kuimba* (*kut15:21, 2nya5:13, 2nya20:21-22, 29:30, Zab9:11, 33:3, 47:6, 66:4, 66:32, 96:1-2, 98:4, 100:2&4, 105:2, 108:1-3, 135:1-3, 147:1, 147:1, 149:1, 6, 150:1, isa12:5, Mndo16:25-26, Efe5:19-20, Kol3:16*)
- *Kusimama* (*2Ny 29:26-31; Zab134:1b, 35:2-3*)
- *Kurukaruka kwa furaha* (*2Sam6:16, Luk6:23, Mndo3:8*)

- *Kupaza sauti (loud voice/noise) (1Nyaya15:28, Zab33:1). Tazama Yesu alivyo shangiliwa alipoelekeea Yerusalem (Lk19:37;Mt21:8-9;Mk11:9) wanafunzi na wafuasi walimsifu Mungu kwa sauti kuu wakisema mbarikiwa mfalme anayekuja kwa jina la Bwana amani mbinguni na utukufu huko juu*
- *Kupiga kelele za shagwe/furaha-joyful noise, vigelegele na kushangilia (Zab5:11,47:1,32:11,33:3,66:1,81:1,95:1-2,98:4,100:1;Yosh6:16,20;Zab35:27, Isa12:6,44:23)*
- *Kucheza mbele za Mungu na si mbele za mwanadamu- hii ni aina ya juu ya kusifu, kudhihirisha furaha -kurukaruka kuinua miguu kama mtu anavyo jisikia (Kut 15:20,2Sam 6:14,6:16,Zab 149:3a,150:4)*
- *Kupiga makofi (Zab 47:1) makofi yapo ya kushangilia na yapo ambayo ni sehemu ya mziki- ni lazima yatofautishwe.*
- *Kuinua mikono juu (Zab 141:2,143:6,1Tim2:8)*
- *Kupeperusha/kushika mikononi vifaa vya kuadhimisha -matawi ya mitende/bendera/vitambaa (Yoh12:13; Ufu7:9; Yer51:12)*
- *Kupiga vyombo vyamziki (2Sam6:5,1Nyak13:8,15:16,19,2Nyak5:12,Zab33:2,108:2,92:3,144:9,149:3,150:3-5,Isa38:20)*
- *Yote hayo kwa ustadi na yaelkezwe kwa Mungu (2Nyaya5:12-14, Zab33:3)*

B. KUABUDU NI NINI? (Zab 95:6-7)

- ❖ Neno abudu (worship) limetafsiriwa kutoka neno la kiebrania [shahah] maana yake ikiwa ni kuinama chini au kuanguka kifudifudi/kusujudu. Kuabudu ni kutoa heshima (pay homage&adoration) ya kiungu anayostahili Mungu.
- ❖ Kutambua kustahili kwa Mungu. Kuabudu ni mwitikio asili (it is a natural response to recognise Who is God, what He has done what He can do) wakutambua kuwa Mungu ni nani na anahusiana vipi na wewe mwanadamu, amefanya nini, atafanya nini n.k. Nguvu za Mungu haziko kwenye vitu, ni kumtambua Mungu na utweza wake. Mfano wa akina Daniel, Meshack, Shadrack na Abednego- (Dan 3:16-28, 6:10-24. Mdo 12:5-7). Petro alilala usingizi (hakuwa na wasiwasi na Mungu wake) akisubiri kutolewa ili auawe kama wenzake. Paulo na Sila badala ya kulia na kuomboleza walimsifu na kumwabudu Mungu (Mndo16:25-28). Shuguli ya kumwadhimisha Mungu, Biblia kw KJV mstari wa 49b inasema [twist ye nothat I must be about my Fathers business]. Rejea ibada za agano la kale kuona ibada ilivyokuwa shuguli (mfano 2Nyaya6:12-14, 7:1-14).
- ❖ Ni ile hali ya kujiachilia kwa heshima ya hali ya juu (adore) kwa mwingine/kitu kingine chenye hadhi ya juu kuliko mtoaji heshima. (art of loosing self in adoration of another). **Kusifu inarweza kuwa ni sehemu ya kuabudu, hata hivyo kuabudu ni Zaidi ya kusifu. Kusifu ni rahisi kuliko kuabudu.**
- ❖ Kumuabudu Mungu kihalisia, kunashitaji mhusika wa kuabudu (mwabudu) kujikana nafsi yake, kujinyenyekenza mbele za Mungu, kujisalimisha nafsi na maisha yake kwa Mungu ili ayatawale na kumwongoza. **Kumtukuza Mungu kwa jinsi alivyo na si kwa sababu tu yale aliyoyatenda au ambayo**

hajatenda kwako. Kuabudu ni mfumo wa maisha na si tukio la mara moja moja (not occasional, it is a life style). Na Mungu anaawataka wamwabuduo **katika Raho na kweli** (Yoh4:23).

- ❖ Wakati kusifu kunahusika Zaidi na furaha (Luk19:37-40), kuabudu Mungu ni tofauti, kuabudu kunahusu mazingira yote kwa kuwa yeye ni Mtakatifu, ni Mkuu Matendo yake yanatisha, nk. (Zab96:9, 95:6).
- ❖ Kuabudu kunaambatana na kuinama/kuinamisha vichwa, kupiga magoti, kusujudia, kusimama, kuonesha unyenyekevu na kujisalimisha kwa Mungu aliye hai (2Nya 7:3-6, 29:28-30, Zab132:7, Heb11:21, Ufu19:10), kuinua mikono juu (Zab134:2, 141:2, 1Tim2:8)

- ❖ Kupitia kuabudu ndivyo kumkaribisha R^oho mtakatifu azungumze nasi, achambue mioyo yetu, atufariji, atukumbushe/atufundishe n.k.
- ❖ Kupitia kuabudu au kusifu au maombi tunampa fursa R^oho Mtakatifu kumwadhimisha Mungu ipasaryo, kutusaidia kuomba na kuzungumza mambo ya ndani ya mioyo kwa lugha zisizotamkika/lugha mpya (**Mndo2:4, 10:46, 19:6, Rom8:26-27, 1kor14:2**). Hivyo ni vizuri kujachilia ili R^oho Mtakatifu achukue nafasi yake, ikiwa ni pamoja na kusifu na kumwadhimisha Mungu kwa lugha mpya kama Mtume Paulo anavyobaini katika **1Kor14:15, 19**, na utaratibu ulioelekezwa **1Kor14:26-33, 39** kulingana na utaratibu usioleta vurugu, mtu anarweza kunena/kuimba kwa akili na katika roho kwa lugha.

KIABUDU-[(kulingana na kitabu cha kanisa la kweli ni lipi?) WORSHIP – is to recognize the worth of God and to give Him honor due to him because of His worthiness] Yaani kutambua kustahili kwa Mungu na kumpa yeye heshima inayomstaili kwa sababu ya kustahili kwake. Hatumwabudu Mungu kwa sababu katutendea kitu fulani, hakuingiliani kabisa na mahitaji na matarajio yetu. Vile tunavyohitaji Mungu akijabudiwa ipasavyo vitakuya kwa kura kwanza sisi ni wa Mungu hata tulivyo navyo na tutakavyopata ni vya Mungu (Yeye ndiye anatupatia nguvu ya utajiri). Ni amana tu (we are stewards-tumewekewa amana kama wawakilishi wa umiliki wa Mungu).

- ❖ Kuabudu ni mawasiliano ya ndani sana kati ya mwanadamu na Mungu, na mawasiliano haya huelezewa kupitia mambo yafuatayo :

- A. Kuadhimisha kwa halii ya juu;
- B. Kutafakari jinsi alivyo wema , fadhilli ,uaminifu wake, matendo yake , nk; (**Zab 117, 130, 136, 138, 145-150**)
- C. Unyenyekevu;
- D. Kujiweka wakfu kwa ajili ya matumizi ya Mungu.

Mambo muhimu au madhihirisho ya kimwili ya kumwabudu Mungu:

- Kuimba/kutamka/kukiri Njoo mbele zake kwa kumwimbia- Zab100:2-5 waliiimba wimbo mpya. (uf5:6)
- Kusimama -Zab134:1b, Zab135:2, **Uf7:9-12** mkutano mkubwa pamoja na malaika wenye uhi wanne na wazee 24 wamesimama mbele za kiti cha enzi na mwana kondoo.
- Kuinua mikono (kjisisalimisha)-Zab134:2, 28:2,143:6
- Kuinama na kupiga magoti-Zab95:6, Fil2:10, **2Nyak 29:30**
- Kuanguka kifudifudi -Uf5:8,14, **Uf4:10-11, Uf7:11-12**
- Kupaza sauti /sauti kuu kumwadhimisha na kuonesha mshangao (**Uf5:12,Uf7:10-wakilia kwa sauti kuu**)

Vitendo vingine vinavyoelezea hisia za mwenye kuabudu kwa Mungu na vinavyoendana na maneno yanayotamkwa mbele za Mungu

3. **KUSIFU NA KUMWABUDU MUNGU**

Kwa nini tusifu na kuabudu?

Makusudi ya Mungu kumuumba mwanadamu ni ili kutawala viumbe (Mwa2:16-17, 19,3:8-11-mahusiano na Mungu-fellowship) Muh12:13,Isay1:19 (kukubali na kumtii Mungu),kumb28:1-4,zab29;2,86:9 (worship-&glorify), 99:5 (exalt-inua/pandisha hadhi -&worship) isay66:23 (wanadamu wote kumwabudu Mungu),Math66:3-utii kwa Mungu). **Kwa jinsi mwanadamu alivyoumbwa hali ya ibada ipo asilia, ama utamwabudu Mungu au shetani** (mwa4:3-4). Aidha, tunasifu na kumwabudu Mungu kwa kuwa tumeagizwa (Zab89:5-6, 103:20, 148:2, Zab138:4,117:1,150:6, Rom15:11).

N.B. Katika kazi zote za kanisa, kazi inayoonekana kuendelea hadi mbinguni ni ya kusifu na kuabudu (Ufu4:8-11)-hivyo kusifu na kuabudu ni shughuli muhimu kwa kila mwamini na ni muhimu ifundishiwe na kupewa nafasi stahiki katika maisha na ibada zetu .

IBADA NI NJINI?

Ibada ni jumla ya mambo yanayofanywa na viumbe (hususani, mwanadamu, malaika n.k.) kutambua na kutoa feshima ya juu, muda na rasilimali kuliko kitu kingine kwa anayestahili kuabudiwa /anayedhaniwa au anayeaminawa kuwa Muumbaji maana hakuna aliye mkuu kuliko Muumbaji. Kwa muktaidha huo, wanadamu wanaweza wasitoe ibada kwa Mungu wa kweli, badala yake ikawa kwa miungu (sanamu, vitu, viumbe wenginwe, shughuli, n.k, **Ikumbukwe kuwa kitu chochote kinachochukwa nafasi ya juu kuliko Mungu ni sanamu-muayu**. Kwa hiyo, ibada ya kweli nijumla ya mambo yote ya mwanadamu yanayomtambua Mungu wa kweli na kumpa feshima na utukufu anaostahili na kumtii amri/maelekezo yake. Ibada hii ni ile iliyofafanuliwa na Bwana Yesu katika **Yoh 4:23-24** kimsingi ibada hii inaanza na mtu binafsi.

4. IBADA YA KUSIFU NA KUABUDU

Ibada ya kusifu na kuabudu ni sehemu ya **IBADA HALISI** (Yoh 4:23), ambapo waabudu wanatamka na kufanya vitendo vya kijibada sawasawa na maandiko. Baadhi ya mambo ya kuzingatia ni pamoja na :Amos 5:21-23 tunatakiwa kuabudu kwa midomo na mioyo (Math 15:8-9, Isay29:13, Mk7:6) ibada ya kusifu na kuabudu ni tukio la wawili au watatu kukusanyika na kumsifu na kumwabudu Mungu sawasawa na maandiko na maelekezo ya Raho Mtakatifu (Math 18:20). Ibada hizi huanza kwa nyimbo za furaha za kumsifu Mungu na kuishia na kipindi cha utulivu kinachomvuta mwabu karibu na mwabuditiwa (kuabudu) yaani Mungu.

Ibada ya kusifu na kuabudu ina marwasiliano ya ndani kati ya mwanadamu na Mungu na inajumuisha unyenyekevu na kujishusha.

Biblia inasema, haki yenu inatakiwa kuzidi ile ya Waandishi na mafarisayo (Math5:20). Mafarisayo walifanya nini katika masuala ya ibada? - walifanya mambo ili waonekane na watu (siyo lazima tushindane na matendo yao -kusali kwa ratiba kwa liturjia ,n.k. ili tuonekane bali tufanye iliyo haki kwa Mungu. Hawa walifanya mambo ya ibada kama Torati ilivyonotaka na mapokeo mengine, kuijhebia haki mbele za Mungu tofauti na yule Mtoza ushuru. Farisayo alitakiwa: (i) aweze kuomba kwa umahiri mbele za watu (Math6:5) (ii) aweze kutumia misamiati na maneno ambayo hayana maana sana lakini yanasiyika vizuri (math6:7) (iii) kipimo cha sala nzuri ilikuwa ni pamoja na urefu wake/maneno mengi (mat6:7) (iv) kuelezea mafanikio

/kujihesabia haki (v) kujilinganisha na wengine mbele za Mungu (LK18:11-12). Hatutakiwi kushindana na wenye dini kimatendo ila Imani yetu (tunachoamini) iendane na matendo. **TUSIFANYE KWA UNAFIKI ILI TUONEKANE NA WATU.**

Kuabudu katika roho na kweli ni **kuongozwa na Roho Mtakatifu**. Wakristo kulingana na Agano Jipyä ni **zadi ya kutekeleza Amri 10**. Kupitia Roho Mtakatifu maelekezo ya Mungu tunayapata katika maisha yote. Yesu hakuja kutangua Torati bali kuitimiza –mfano usiue - hata ukimchukia ndugu yako u muuaji usizini – hata ukitamani umesha zini moyoni n.k. (Mat5:17-48).

Kuabudu ni shughuli (business/activity) ya Mungu, rejea ibada za agano la kale watu walivyo shughulika /walivyomwabudu Mungu (**Mfano 2Nya5:7,12,13**).

Ibada inatakiwa iwapeleke watu kwenye uwepo wa Bwana, ibada ya kweli Mungu anashuka na mwabudu anapanda hadi kikutana na Mungu (Zab22:3, **Mdo16:25-29**). Mungu anakaa kwenye sifa. **Mwongozaji hana haja ya kuwaelekeza watu cha kufanya** – kila mtu anfanya anachosukumwa na Roho kufanya – kifudifudi, kupiga magoti, kusimama na kuinua mikono juu, kuinamisha kichwa chini n.k.

Hitimisho la ibada ya kusifu na /au kuabudu ni Mungu kushuka mwenyewe –madhirisho ya uwepo wa Mungu, Mungu anafanya yeye mwenyewe mambo kama vile uponyaji, miujiza, pepo wanatoka wenyewe, majibu ya maombi n.k. Mfano ni:

- 1Sam19:18-24 Nayothei ya Rama ibada ilishusha uwepo wa Mungu, **MUNGU ALISHUKA NA KUKAMATA MADUI** ikiwa ni pamoja na mfalme Sauli.
- 2Nya5:14 -makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma kwa sababu ya uwepo wa utukufu wa Mungu ambao unafukuza kila kilicho cha shetani. **Maaskofu na wachungaji wanakuwa na kazi ndogo kama Roho akishuka na kuongoza**, na kila mwamini akiwa kwenye uwepo wa Mungu.

Kila mwabudu anatakiwa kujianaa mapema kwa ibada ya kusifu na kuabudu.

5. **MPANGILIO WA SALA/IBADA KWA KULEJEA SALA YA BWANA** (Mat6:8-13)

Mambo yote yanatakiwa kwa utaratibu (1Kor14:40) kama ilivyo kwenye mwongozo aliotoa Bwana Yesu Kristo kwenye Mt 6:8-12. Anza na kusifu/kutukuzza (**baba yetu uliye mbinguni jina lako litukuzwe**) tenga muda wa ukimya/utulivu kumpa mungu/roho nafasi ya kunena naue au kusanyiko (Zab37:7,62:1, Zek2:13).

Aidha mambo yafuatayo ni mufimu kuzingatiwa:

- Ulimbaji/ustadi – mpangilio wa sauti, vyombo na mtiririko – sifa hadi kuabudu bila kukatishakatisha (seamless) – acha muda wa utulivu - kuka kimya mbele za Bwana – ruhusu Mungu kuongea na miyojo ya waabudu (Zab37:7,62:1, Zek2:13)
- Vitendo vya kusifu na kuabudu kama viliyvo elezwa hapo juu: kuimba, kunena/kusema, kuinua mikono juu, kuinama, kusujudu, kuanguka kifudifudi, n.k.
- Ukimya na tafakari na kusikiliza iwapo Mungu ana cha kuongea.

6. MAMBO MUHIMU KWENYE IBADA YA KUSIFU NA KUABUDU


- i. Mwabudiwa ni Mungu hivyo nyimbo zichaguliwe /zitungwe vizuri ili kumenga Mungu moja kwa moja na kumsaidia mwabudu/mwimbaji kumwimbia Mungu moja kwa moja kutoka kwenye nafsi yake.

MFANO KWENYE KUSIFU:

- Pokea sifa Bwana heshima utukufu nakupa wewe/Siyo heshima utukufu twakupa wewe
- Ee Yahwe usifiwe/Siyo Ee Yahwe asifiwe
- Umetenda mema ndiyo maana leo ninakutukuzza/Siyo ametenda mema ndiyo maana leo tunakutukuzza
- Ninakusifu Mungu wangu ninakusifu wewe ni Bwana/siyo tunakusifu Mungu wetu

KUABUDU

- Wasitahili sifa za Moyo wangu/Siyo sifa za mioyo yetu
 - Baba nina kuabudu/Siyo tunakuabudu
 - Ee Mungu wangu ninakuabudu/Siyo ee Mungu wetu tunakuabudu
 - Ukimya (Be still in the presence of the lord, and wait patiently for him to act-Zab37:7a, 62:1, Zek2:13-kuacha nafasi kama Mungu ana ujumbe maalumu kwa ajili ya kusanyiko).
- ii. Kiongozi /Viongozi awe katika halii ya kuwaunganisha waabudu na Mwabudiwa na si kuwaondoa wanaoabudu kutoka kwa Mungu. Hivyo, mwonekano wao, nyimbo na mtiririko vikae vizuri. **Mtiririko usikatishwekatishwe, ama kwa maneno ya kiongozi au vyombvo vya mziki.**
- iii. Nyimbo ziimbwe zinazofahamika na waabudu walio wengi hasa pambio. Kama ni lazima nyimbo au pambio mpya ziimbwe, ziwe zenye maneno machache yanayoweza kufuatwa na waabudu kwa haraka na hivyo kutosumbua uwepo wao mbele za Mungu. Rejea kama vile, vitabu vya nyimbo au/na maandishi yanayosomeka na wote (ukutani au ubaoni). Vinaweza kuboresha mwitikio na utulivu /uhuru wa kuabudu. Kunatakiwa kutwa muunganiko (connection) nzuri kati ya wahusika wote (Rejea kielelezo).



7. WASIFU (SIFA) WA ANAYESIFU NA KUMWABUDU MUNGU

Awe anatimiza makusudi ya Mungu kumuumba mwanadamu yaani kutawala viumbwe (mwa1:26) na kumcha Mungu kwa kushika amri zake na kumwabudu (Muh12:13, Kumb26:1-4, Mat6:33). Kwa hiyo Mwabudiwa (Mungu) ahusike ipasavyo. Mwenye kumsifu na kumwabudu Mungu ikiwa ni pamoja na kiongozi wa ibada ya kusifu na kuabudu anatakiwa awe wa Bwana /aliyekombolewa (Law27:28, Zab107:1-2, Kut15:1-21) na

ameokoka vizuri – amempokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake na amemkataa shetani na mambo yake yote (Mk16:16, Yak4:7, Kol 1:13, Yoh1:12). Kwa hivyo, anyemwabudu Mungu anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- 1) Anakiroho kizuri/ameokoka vizuri –(Yoh4:23, Yak2:19)
- 2) Awe na kiu ya kumjua Mungu –msomaji wa Neno, mwombaji, mshuhudiaji na anaukulia wokovu (1Pet2:2, Mith8:17-kumtafuta Mungu kwa bidii)
- 3) Awe na twito (1Kor12:28-maongozi, Efe4:11-15, kila kiungo kufanya kazi yake ,Mith17:8-kipawa/kito cha thamani)
- 4) Ajitoe sadaka (sacrifice) (Rom12:1)/Moyo safi ,mikono safi ,unyofu wa moyo –Zab.24:3-4, 33:1, 51:17, Isa57:15,66:26 ,
- 5) Aishi maisha matakatifu (hana udunia wala haleti udunia kwenye ibada)-Mtakatifu /aliyetakaswa/mtauwa –Zab149:5, Ebr13:15, Yoh13:3-10, 1Yoh1:9.
- 6) Dhamiri safi –Ebr10:22
- 7) Unyenyekevu –Zab89:7
- 8) Mavazi ya wokovu (si uchi)-Zab132:16, 1Kor3:16-17
- 9) Aliye tiwa mafuta /waliojazwa Roho Mtakatifu-Yoh 4:23,Ef2:18,5:18-19
- 10) Awe na mandalizi ya ibada na ya huduma (kuandaa nyimbo,kufanya mazoezi ,mavazi ya stahia /heshima ,sadaka ,maombi n.k.)
- 11) Awe mtu wa kuwahi na kutunza muda kwenye matukio hususani ambayo Mungu ameahidi kuwapa (Mat18:20), kukomboa wakati (Ef5:16,kol4:5)
- 12) Aimbe na /au kupiga vyombo kwa ujasiri /kujiamini na ustadi.

Kimsing, Anaye sifu awe ameokoka vizuri –mtakatifu (Zab16:3)

Ipo haja ya kujifunza na kuendeleza kusifu na kuabudu kwa kuzingatia wasifu ulioelezwa hapo juu.

8. MASHARTI YA IBADA YA KUSIFU NA KUABUDU KUKAMILIKA

Ili ibada ya sifa na kuabudu ikamilke inahitaji uwepo wa:

- 1) Anayeabuditwa (Yoh1:1-3, Yoh4;20-23)-Mungu
- 2) Anaye/wanao-abudu-(Yoh4:23)
- 3) Vitendea kazi vya ibada –vyombo vya mziki, utoaji wa sadaka (1Nya16:29, Kumb 16:16-usitokee mbele za Bwana mikono mitupu).

9. UCHAGUZI WA NYIMBO ZA IBADA

Kwa kuzingatia uelewa unaotokana na somo hili jedwali lifuatalo litoa mwanga wa aina ya nyimbo na wakati/mahali zinapotakiwa kuimbwa /kutumika:

10. VIONGOZI WASIFA NA KUABUDU

Viongozi wa ibada ya sifa na kuabudu ni Zaidi ya mwimbishaji hawa ni watu wenye sifa zilizotajwa na wanatambua kazi yao muhimu ya kuwaunganisha watu na Mwabudiwa.

Viongozi wanawenza kuwa:

- 1) *Mtu mmoja mmoja (individuals).*
- 2) *Kikundi cha waimbaji (1Nyaya15:16-29, 2Nyaya5:12-13). Timu ya sifa na kuabudu na /au kwaya. Katika 1Nyaya16:7-36 kundi husika lilifanya huduma kikwaya na lilifanya kazi ya kukumbushana matendo makuu ya Mungu na kuhamasisha watu kumwabudu na kumwadhimisha Mungu aliye hai (3rd person na sio one to one with God) ndipo hitimisho likawa watu kumhimidi Bwana.*

11. AINA ZA KUSIFU NA KUABUDU KWA VITENDO

Baadhi ya vitendo viliyo tumirwa na watu wa Mungu hasa katika agano la kale na badhi yake hutumiwa na madhehebu/watu wa Imani mbalimbali hata sasa katika Agano Jipya vimeorodhesiwa hapa chini. Kwakuwa tulio kombolewa kwa damu ya Bwana Yesu, sheria ya Bwana imo miyoni mwetu na kiyango chetu inabidi iwe Zaidi ya torati tukiongozwa na Raho Mtakatifu, vipo vitendo kati ya viliyo tajwa ambavyo ni muafaka kurifanya kwa hiari yetu, vitendo vingi vinaonekana kufanyika mbinguni (Uf 7:9-12).

1. **Barak**-kuinama chini mbele ya mwabudiwa, kupiga magoti mbele za Bwana, kusujudu(adore) kuonyesha unyenyekevu na kutambua ukuu wa Mungu; (Zab22:27, 66:4, 72:12-15, 103, Isa45:23, Rom14:11, Fil2:10-11, Uf5:13).
2. **Hallał**-kutoa sauti dhahili kusheherekeea, kusifia sana/adhimisha (exalt), kutukuzza (magnify), kujidai (1Nyaya16:4, 23:5, Zab 34:3, 40:16)
3. **Hiluwi** – sherehe ya kutoa shukurani ya mavuno –uchanafu kuchenza Zab 150:4-5.
4. **Tehillah**-kuimba nyimbo waziwazi bila mazoea ya awali, kusifu ambako hakukua kumepangwa (Zab34:1, 40:6).
5. **Shabach** - kupiga kelele au amua kwa sauti ya shangwe njia muhimu ya kumsifu Mungu Zab 47:1 (Makofit) Zab63:1-4.
6. **Towdah** - kujunjua mikono au kujinua mikono katika kushukuru kwa ajili ya yaliyotokea au ambayo hayajapokelewa (kwa Imani) Zab50:23, Yer17:26
7. **Yadah** - ukri wa shukrani kujunjua mikono mbele/juu kwa nguvu kama anayejisalimisha (2Nyaya20:21, Zab9:1)
8. **Zamat/Zamar** - kupiga /kuchenza vifaa vya muziki (ala) +kinanda cha nyuzi 10 (Makofit)(zab92:1-3,150,

9. **Kuabudu** – ni kuonyesha heshima,kuwa na kicho/hofu ya Mungu ,kuinama chini mbele ya kitu kinachopewa heshima ya hali ya juu (Mungu) pamoja na kusujudu (zab66:4)

12. HITIMISHO

Kusifu na kumtwabudu Mungu ni sehemu ya ibada halisi (Yoh4:23) na inahusu kuishi sawasawa na mapenzi ya Mungu ikiwa ni pamoja na kutoa mili yetu iwe dhabihi /sadaka iliyo hai (kumpendeza Mungu). Ibada ya kusifu na kuabudu ni shughuli pekee kati ya zilizopo hapa duniani itakayoendelea milele na milele kama tunavyoona kwenvye maandiko. Hivyo, kujifunza/kujikumbusha na kutekeleza ipasavyo shughuli hii ni muhimu. Ni vema somo hili liwe sehemu ya mambo muhimu ya kanisa kufundisha na kutekeleza chini ya uongozi wa Raho mtakatifu.